# MTIHANI WA DARASA LA TANO MUHULA WA PILI 2018 KISWAHILI

*Muda: Saa 1 dakika 40*

***Soma vifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa kuanzia 1 - 15.***

Hospitalini ni mahali ____1____ kuwatibu watu ____2____ magonjwa mbalimbali. Hospitali ____3____ huitwa ____4____ au kituo ____5____ afya. Daktari na mwuguzi hupatikana ____6____ hospitali. ____7____ ndio huwatibu wagonjwa. Vyumba vya ____8____ wagonjwa huitwa ____9____. Vifaa ____10____ hospitalini huwa safi sana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. ya | B. pa | C. yenye | D. wa |
| 2. | A. yenye | B. zenye | C. wenye | D. mwenye |
| 3. | A. ndogo | B. kidogo | C. mdomo | D. dogo |
| 4. | A. bweni | B. nyumba | C. zahanati | D. chekechea |
| 5. | A. cha | B. wa | C. ya | D. za |
| 6. | A. ma | B. katika | C. ndani | D. kwa |
| 7. | A. Nyingi | B. Huyo | C. yeye | D. wao |
| 8. | A. kuweka | B. kuwalea | C. kulia | D. kuwalaza |
| 9. | A. kodi | B. chumba | C. wodi | D. darasa |
| 10. | A. vya | B. la | C. za | D. wa |

____11____ magari matano ____12____ ukipita kwa utaratibu ambapo watu walisimama ____13____ barabara wakiyatazama magari ____14____ kwa makini mno ____15____ jinsi yaliyopambwa kwa maua kochokocho.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 11. | A. Safari ya | B. umati wa | C. safu ya | D. mlolongo wa |
| 12. | A. walikuwa | B. tulikuwa | C. ulikuwa | D. ilikuwa |
| 13. | A. mbele ya | B. kando ya | C. mkabala wa | D. nyuma ya |
| 14. | A. hayo | B. hiyo | C. hizo | D. zile |
| 15. | A. wakipenda | B. wakifurahika | C. wakishangaa | D. wakifurahia |

***Kutoka swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.***

16. Akisami $\frac{1}{3}$ kwa maneno ni
A. humusi
B. subui
C. thuluthi
D. sudusi

17. Kamilisha methali hii
**Mvumilivu hula**
A. mbivu
B. mbichi
C. tamu
D. yote

18. Umbo hili huitwa



A. pia
B. mstatili
C. mche
D. pembe tatu

19. Tumia kiashiria kinachofaa
**Gurudumu _____ la gari limetoboka**
A. huu
B. hii
C. huyu
D. hili

20. Andika tarakimu hii kwa maneno 6969.
A. Elfu sita mia tisa sitini na tisa
B. Elfu tisa mia sita sitini na tisa
C. Elfu tisa mia sita tisini na sita
D. Elfu sita mia sita sitini na sita

21. Tegua kitendawili hiki
**Mzee mwenye kabuti la chumba**
A. ndovu
B. kondoo
C. kobe
D. macho

22. Maamkizi; Alamsiki hujibiwaje?
A. Binuru
B. Alamsiki
C. Buriani
D. Biuru

23. Jiko la makaa huitwa
A. gesi
B. stovu
C. meko
D. seredani

24. Kanusha
**Mwalimu anafunza kwa utaratibu**
A. Mwalimu anasoma kwa utaratibu
B. Mwalimu hafunzi kwa utaratibu
C. Mwalimu afundisha kwa utaratibu
D. Mwalimu anasoma kwa utaratibu

25. Kinyume cha masika ni
A. ukame
B. kipupwe
C. kiangazi
D. njaa

26. Ndege huyu ni wa mtu _____?
A. upi
B. gani
C. kipi
D. mgani

27. Mbona unakula ugali _____ kitoweo
A. bila
B. na
C. lakini
D. mbali

28. Mtoto _____ ni huyu
A. angeoga
B. ahoga
C. aliyeoga
D. ataoga

29. Sisi _____ kikazi cha viongozi wa kesho
A. ndisi
B. ndio
C. ndivyo
D. ndiye

30. Joto _____ husababisha maradhi
A. mingi
B. jingi
C. kingi
D. mengi

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Hapo zamani za kale palikuwa na insi mmoja ambaye kazi yake ilikuwa kutema kuni. Alikuwa na wana watatu, wawili wa kike na mmoja wa kiume. Kila mara alipotoka kutema kuni, alikuwa akimpiga mkewe kwa makosa madogo madogo. Kwa ukatili huu mkewe akawaza kuwa siku moja angelipisha kisasi.

Katika nchi hiyo kulikuwa na mfalme ambaye hakuwa na furaha hata kidogo kwa sababu bibi yake alikuwa bubu. Alijaribu kutafuta mganga asimpate. Siku moja aliwatuma askari wake waende wakatafute mganga. Baada ya safari ndefu, walifika kwa mtema kuni. Walimwuliza mkewe kama anajua mganga yeyote ambaye anaweza kumtibu bintiye mfalme.

Alisema eti mumewe ni mganga wa miti shamba na ako msituni akitafuta majani, mizizi na matunda ya kutengeneza dawa, lakini asipopigwa sawasawa husema yeye si mganga kazi yake ni kutema kuni.

31. Mtema kuni alikuwa na banati wangapi?
   - A. Wawili
   - B. Watano
   - C. Mmoja
   - D. Watatu

32. Bidhaa Mtema kuni alitafuta msituni husaidia aje nyumbani?
   - A. Kupika
   - B. Dawa
   - C. Kuadhibu
   - D. Shambani

33. Mtema kuni aliishi wakati gani?
   - A. Wakati kale aliishi
   - B. Miaka miwili iliyopita
   - C. Wakati zama na kale waliishi
   - D. Miaka mingi iliyopita

34. Mfalme alikuwa amehuzunika kwa sababu bintiye alikuwa
   - A. haoni
   - B. hatembei
   - C. haongei
   - D. hasikii

35. Kulingana na familia ya Mtema kuni ni kazi ipi nyingine angeweza kufanya?
   - A. Kutema kuni
   - B. Kuchapa bibi
   - C. Kutibu
   - D. Kuuza

36. Kulingana na habari ni sehemu ipi ya mti haitumiki kutengeneza dawa?
   - A. Majani
   - B. Matunda
   - C. Shina
   - D. Mizizi

37. Ni kweli kusema Mtema kuni alikuwa mganga?
   - A. La
   - B. Itategemea
   - C. Ndio
   - D. Hatujaambiwa

38. Ili Mtema kuni akubali kumtibu bintiye mfalme angefanywa nini?
   - A. Kuchapwa
   - B. Kuongea
   - C. Kutengeneza dawa
   - D. Kunawa

39. Kama malipo yake, angelipwa nini baada ya matibabu?
   - A. Nauli
   - B. Kiinua mgongo
   - C. Mshahara
   - D. Ada

40. Ni sifa gani ambayo mzee Mtema kuni alikuwa nayo kulingana na habari?
   - A. Mnene
   - B. Mvumilivu
   - C. Mkaidi
   - D. Hodari

*Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.*

Tangu asili ya jadi, mwanadamu huishi kusafiri. Ziara husababishwa na mambo mengi. Ama mwanadamu hutafut chakula, hutembelea familia yake, hutafuta kazi itakayompatia riziki au hata kutafutia wanyama wake malisho.

Safari za zamani zilikuwa ngumu. Watu walipiga milundi, wakipitia katika nyika na hata sehemu nyinginez zenye hatari kama vile misitu yenye wanyama wakali.

Siku hizi mambo yamebadilika. Aina mbalimbali za usafiri zinapatikana. Kuna usafiri wa nchi kavu, ule wa majini na hata usafiri wa nchi angani. Katika nchi kavu tuna barabara za magari ya aina mbalimbali. Magari madog ambayo hapa nchini Kenya huitwa "matatu" yanatumiwa sana mijini. Abiria hupanda na kulipa nauli wakiwa safarini.

41. Mwandishi ametaja aina ngapi za usafiri?
A. Saba
B. Mbili
C. Tatu
D. Nne

42. Jambo moja linalomfanya mwanadamu asafiri ni
A. kuiba
B. kucheza
C. kutafuta chakula
D. kutembea tu

43. Kupiga milundi ni
A. kuruka
B. kuketi
C. kulala
D. kutembea

44. Abiria anaposafiri hulipa
A. nauli
B. gharama
C. kodi
D. faini

45. Safari za zamani zilikuwa hatari kwa sababu ya
A. urefu
B. mito
C. barabara
D. wanyama wakali

46. Ukitaka kusafiri nchi za Ulaya utatumia
A. miguu
B. gari
C. ndege
D. pikipiki

47. Magari ambayo hutumika sana mijini ya Kenya ni
A. rukwama
B. bodaboda
C. mikokoteni
D. matatu

48. Riziki ni
A. hati ya kusafiri
B. nyimbo
C. tikiti
D. chakula

49. Anayesafiri majini atatumia
A. meli
B. matwana
C. tuktuk
D. ndege

50. Anayetafutia wanyama malisho ni
A. mchungaji
B. mtabiri
C. mkulima
D. daktari wa mifugo